**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO : GA.71/135/EZ/2024/01**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000023**

**KATI YA**

**CI-GROUP LTD ........................................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA**
**(TANESCO)........................................................................ MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 146 cha tarehe 17 mwezi Machi 2025)***

## 1. Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 23 Januari 2025, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa C.I. Group ikiwakilishwa na Saulo Jackson Kusakalah wa Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam (Mlalamikaji) dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) (Mlalamikiwa). Mlalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kumtoza ankara isiyo halali kiasi cha TZS 78,289,797.30.

Mlalamikaji anaeleza mnamo tarehe 23 Januari 2023 maofisa kutoka ofisi ya Mlalamikiwa walifika eneo la Mlalamikaji kwa ajili ya ukaguzi wa miundombinu ya umeme walipofika walienda moja kwa moja katika dira ya umeme kwa ajili ya uchunguzi. Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba mara ya baada kumaliza uchunguzi wao walimpatia taarifa kuwa nyaya ndani ya dira hiyo zimefungwa tofauti na hivyo imesababisha upotevu wa umeme katika upande wa matumizi.

Mlalamikaji anafahamisha kwamba mnamo tarehe 25 Februari 2023 alipokea barua kutoka ofisi ya Mlalamikiwa ikitoa taarifa juu ya ukaguzi ambao umefanyika tarehe 23 Januari 2023, na kumtaka Mlalamikaji alipie kiasi bishaniwa cha TZS 78,289,678.35 ikiwa ni gharama ya umeme uliopotea katika matumizi yake baada ya nyaya za dira kufungwa tofauti.

Mlalamikaji anaendelea kufahamisha kwamba waliendelea kufanya mawasiliano na ofisi ya Mlalamikiwa kwa kuandika barua tarehe 27 Machi 2023 ya kupinga madai ya TZS 78,289,678.35 yaliyowasilishwa kwa barua ya tarehe 25 Februari 2023 kutoka kwa Mlalamikiwa. Mlalamikaji anafafanua kwamba yeye alikuaamekwishalipa ankara zote za miezi yote bila kuacha, hivyo Mlalamikiwa hapaswi kumdai Mlalamikaji kwa maana ni makosa ambayo yamesababishwa na wao wenyewe na sio makosa ya Mlalamikaji.

Mlalamikaji anaendelea kufafanua zaidi kwamba alifanya mawasiliano na Mlalamikiwa kwa muda mrefu sana na kuomba Mlalamikiwa aandike barua ya kutoendelea kuidai ofisi yake lakini hakupata muafaka wa malalamiko yake, mnamo tarehe 23 Januari 2024 Mlalamikaji aliwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka (EWURA) na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa mambo yafuatayo: -

(a) Kuondolewa kwa deni bishaniwa kiasi cha TZS 78,289,678.35 kwenye akaunti ya Mlalamikaji.

(b) Mlalamikiwa asifanye chochote juu ya huduma inayotolewa kwa Mlalamikaji hadi pale Malalamiko yatakapofikia muafaka.

Baada ya kupokea malalamiko ya Mlalamikaji, Mamlaka (EWURA) mnamo tarehe 29 Januari 2024, ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuleta waraka wa utetezi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za utatuzi wa Migogoro (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure*), Rules 2020)).

Mnamo tarehe 20 Februari 2024, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kueleza kwamba dira ya Mlalamikaji ilikuwa inahesabu chini ya kiwango na hivyo Mlalamikaji anapaswa kulipia kiasi cha TZS 78,289,678.35 kwani ni matumizi yake ya umeme ambayo alikuwa anayatumia.

Mlalamikiwa anaendelea kueleza kwamba Mlalamikaji anapswa pia kuthibitisha Malalamiko yake na madai mengine yote ambayo ameorodhesha katika fomu yake ya Malalamiko, anaendelea kueleza kwamba anaiomba Mamlaka (EWURA) kutupilia mbali Malalamiko ya Mlalamikaji kwa kuwa hayana msingi wowote ule.

Vikao vya usuluhishi baina ya pande zote mbili vilifanyika tarehe 21 Mei 2024,tarehe 12 Novemba 2024 na tarehe 14 Februari 2025 katika ofisi za Mamalaka (EWURA) jengo la Psssf Complex Ghorofa ya nne mwisho wa kikao wadaawa walikubaliana mambo yafuatayo:-

(a) Mlalamikaji atalipa kiasi bishaniwa cha TZS 78,289,797.30 bila riba katika kipindi cha miezi 24 kuanzia tarehe 14 Februari 2025 hadi tarehe 15 februari 2027 kwa malipo ya TZS 3,262,074.89 kila mwezi; na

(b) Mlalamikiwa atafuta riba zote zitakazotokana na kiasi bishaniwa cha TZS 78,289,797.30 mara baada Mlalamikaji atakapomaliza kulipa kiasi cha TZS 78,289,797.30.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali Na. 428 la 2020 na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

**2. Makubaliano**

Pande zote mbili zilikubaliana yafuatayo:-

(a) Kwamba Mlalamikaji atalipa kiasi bishaniwa cha TZS 78,289,797.30 bila riba katika kipindi cha miezi 24 kuanzia tarehe 14 Februari 2025 hadi tarehe 15 Februari 2027, kwa malipo ya tzs 3,262,074.89 kila mwezi; na

(b) Kwamba Mlalamikiwa atafuta riba zote zitakazotokana na kiasi bishaniwa cha TZS 78,289,797,30, mara baada mlalamikaji atakapomaliza kulipa kiasi cha TZS 78,289,797.30.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali namba 428 la 2020, makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Dodoma tarehe 17 mwezi Machi 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**